



**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TISA**

**Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 28 Februari, 2018.**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi  
na Dua itasomwa.

**MASWALI:**

**Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:**

56. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) -  
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji,  
Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:

Kwa kuwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee,  
Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka wa fedha  
2016/2017 ilijipangia kukusanya Tshs. 487,400,000/=  
lakini hadi kumaliza kwa kipindi hicho, Wizara  
haikukamilisha lengo la makusanyo hayo. Kwa  
mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara imejipangia  
kukusanya jumla ya Tshs. 891,078,000/= ambapo ni  
sawa na ongezeko la Tshs. 403,678,000/=.

- (a) Je, hadi kufikia mwezi Disemba 2017, Wizara  
kupitia Taasisi zake imeshakusanya kiasi gani  
cha fedha kwenye malengo yake iliyojipangia.
- (b) Je, hadi kufikia mwezi Disemba 2017, ni  
mikataba mingapi ya ajira za nje, vibali vya

kazi kwa wageni, vimetolewa na ni vyama vingapi vya ushirika ambavyo vimesajiliwa.

- (c) Je, hadi sasa ni upi mwelekeo wa Wizara hiyo kuhusu kufikia lengo la makusanyo ambayo Wizara kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 2018 umejipangia.

**Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:**

- 60. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHANI SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

Pamoja na jitihada za Serikali kuendeleza michezo ya aina zote, na kuleta mafanikio kama tulivyofanikiwa katika mashindano ya CECAFA, yapo baadhi ya mambo ambayo tunatakiwa kujipanga ili kuleta mafanikio zaidi.

- (a) Je, Serikali imejipangaje kwa wanamichezo kuwapima afya zao na uwekaji wa kambi za mazoezi ya kimashindano.
- (b) Kuna matamasha mengi yanayofanyika Zanzibar kama tamasha la nchi za jahazi na mengineyo lakini kwanini matamasha haya sijawahi kuona kilele kikafanyika Pemba.

- 67. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHANI SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

Mafanikio ya timu ya Zanzibar iliyoyapata katika mashindano ya CECAFA pamoja na kitendo cha Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwatunukia zawadi wachezaji hao, imeleta hamasa kubwa kwa vijana wetu kupenda michezo.

- (a) Je, Serikali imejipanga vipi kuwawekea watoto maeneo ya kuchezea mipira katika maeneo ya miji mikongwe na miji mipya.

- (b) Je, yako wapi maeneo ya viwanja katika miji ya plani kama Mombasa kwa Mchina, Mpendae, Chukwani na maeneo kama hayo.
- (c) Je, suala la viwanja vya michezo katika maeneo kama hayo hayakuzingatiwa na kama yalizingatiwa yako wapi.

**Wizara ya Afya:**

52. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) -  
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa madaktari kutoka Hospitali ya Miot ya nchini India ambayo ndipo tunapopeleka wagonjwa wetu wengi kwa matibabu mbalimbali walikuja hapa nchini kwa ajili ya kutoa huduma za kutibu wagonjwa. Na kwa kuwa kabla ya ujio wao kulikuwa na wagonjwa ambao walipaswa kupelekwa huko India kwa ajili ya matibabu.

- (a) Je, ujio wa madaktari hao wameokoa kiasi gani cha fedha ambacho kingetumika kwa kupeleka wagonjwa wetu huko India.
- (b) Je, madaktari hao waliweza kuhudumia wagonjwa wangapi.
- (c) Je, madaktari hao waliwatibu maradhi gani.

Zanzibar,  
28 Februari, 2018.

**(Raya Issa Msellem)**  
**KATIBU WA BARAZA.**